Wataalamu hawa walidai kuwa nomino mahususi huundwa kwa mizizi tu na haziwezi kuchanganuliwa

*Corresponding Author: David Micheni Mutegi


Tharaka University, P. O.Box. 193 Marimanti, Kenya

kimofolojia, madai yaliyoungwa mkono na Karanja na Habwe (2007) walioshikilia kuwa nomino za pekee kama vile za mahali hujidhihirisha katika maumbo yake maalum.

Uchunguzi pia umefanywa kuhusiana na mbinu za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili ambazo zinasaidia kuzalisha maumbo ya maneno. Mbinu hizo ni pamoja na unyambuaji, ufupishaji, ukopaji, uhulutishaji na mwambatano. Kahigi, (2007) anaongeza mbinu ya eponimu inayohusu utoaji wa majina ya mahali kutokana na majina ya watu. Massamba, (2004) aliongeza mbinu ya uhamishaji maana inayohusisha maneno ambayo tayari yanatumika katika lugha inayohusika kwa kupewa maana mpya.

Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu majina kwa jumla. Musyimi, (2011) alichunguza maana, ishara maana na misingi ya kitamaduni ya majina ya watu katika jamii ya Wakamba. Aligundua kuwa kulikuwepo na majina mengine kama ya mahali, ya mito na wanyama lakini mipaka ya utafti wake haikumruhusu kuyashughulikia. Masanja, (2019) alifanya utafiti uliohusu uchunguzi wa kisemantiki wa majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Utafiti wake ulionyesha vigezo vinavyotumiwa katika kuteua majina ya asili na kubainisha miktadha ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Fatma, (2018) alichunguza namna majina ya watu mashuhuri yalivyotumika katika kutoa majina ya Wapemba.

Ingawa kipengele cha majina kinaonekana kushughulikiwa na wanaisimu mbalimbali kama ilivyofafanuliwa, utafiti uliofanywa ulishughulikia zaidi semantiki ya majina ya watu na mahali bila kushughulikia kwa kina suala la vigezo vya utoaji wa toponemia katika jamii. Uhaba wa utafiti wa aina hii ulifanya jamii kupungukiwa na maarifa muhimu kuhusu maana na asili ya toponemia katika jamii zao. Utafiti huu ulilenga kufidia pengo hili kwa kuchanganua vigezo vya utoaji wa toponemia za shule za msingi katika jamii za Wamwimbi na Wamuthambi.

**MWAUO WA MAANDISHI**

Utafiti wa majina ya watu uliofanywa na Guma, (2001) katika jamii ya Basotho wa Afrika Kusini ulibaini kuwa jina ni zaidi ya neno au maneno yanayomtambulisha mtu. Mtafiti huyu alidai kwamba utoaji wa majina ni tukio la kijamii na kiutamaduni lililoonyesha historia ya jamii. Kulingana naye, majina husimamia tajiriba ya mtu au kikundi cha watu, mila, desturi, hadhi na mamlaka katika jamii. Pamoja na kuwa utafiti huu ulibaini kuwa jina ni zaidi ya maneno yaliyomtambulisha mtu, kulikuwa na haja ya kuchunguza vipengele vingine vilivyohusiana na majina kama vigezo vya utoaji wa toponemia.

Wanaisimu Rubanza (2000), Mphande (2006) na Manyasa (2009) walichunguza na kufafanua maana za majina na muktadha unaochochea uteuzi wa majina ya watu katika jamii za Kiafrika. Wataalam hawa walisisitiza kwamba, maana ya majina ya watu hutegemea kusudi la mtoa jina na miktadha. Kwa kuzingatia ubunifu, kama ilivyo katika lugha nyingine za Kibantu, majina ya watu huwa na maana mahsusi. Maana hiyo hutegemea mazingira alimozaliwa mtoto, hitaji la kuendeleza kizazi, migogoro na malumbano ya kifamilia au kijamii. Tofauti na utafiti wa wataalamu hawa (washatajwa), utafiti huu ulichunguza vigezo vya utoaji wa toponemia katika jamii.

Werner-Lewis (2003) alitafiti kuhusu majina ya watu katika jamii lugha ya Afrika ya Kati. Lengo la utafiti wake lilikuwa kutafiti majina na maana zake. Utafiti huo alibaini kuwa majina hayatolewi kiholela katika jamii lugha husika bali utoaji wa majina hufuata kanuni na taratibu za jamii husika. Aliendelea kueleza kuwa maana za majina hufungamana na tabia za watu, utamaduni, matukio na hali zinazojitokeza wakati wa kuzaliwa kwa mtoto. Ingawa utafiti huu ulichunguza majina ya watu, ulimsaidia mtafiti kiasi kwani ulibainisha kuwa toponemia hazikutolewa kiholela bali palizingatiwa vigezo maalum.

Utafiti wa majina ya watu uliofanywa na Musere (2010) katika jamii ya Wabaganda nchini Uganda ulibainisha kwamba majina mengi ya watu katika jamii hiyo yalinasibishwa na methali. Musere (keshatajwa) anaeleza kuwa jina hunasibishwa na heshima fulani kwa kuzingatia vigezo vya kiakili, urafiki, ushirikiano, shukrani, utoaji, ujinga na kusifu. Katika kushadidia hoja yake, Musere (keshatajwa) alitoa majina yatokanayo na methali kama vile "*Ebigambo tebyasa (tibyasa) mutwe,*" yaani maneno hayapasui kichwa. Kutokana na methali hiyo mtu anaweza kuitwa Tebyasa. Maelezo haya ni muhimu kwani utafiti huu ulishughulikia majina ya mahali kwa kuchunguza vigezo vilivyotumiwa katika kutoa toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi.

Baitani (2010) alichochewa kutafiti kutokana na utafiti wa Rubanza (2000) uliokuwa na upungufu kutokana na uchache wa data zilizotumika na makosa mengine ya kimaumbo. Katika utafiti huo ilibainika kuwa, kama ilivyo katika lugha nyingine za Kibantu, majina ya Kihaya yana maana inayoakisi maisha na mazingira ya jamii yao. Hivyo utafiti huo ulisaidia mtafiti kubainisha vigezo vya kijamii na kimazingira vilivyochangia katika utoaji wa toponemia katika jamii.

Nyanganywa (2013) alifanya utafiti kuhusu majina ya watu katika jamii ya Wajita nchini Tanzania. Katika utafiti huo mtafiti alifanya uchunguzi wa kisemantiki na taratibu za utoaji wa majina ya Kijita na kubaini kuwa majina ya Kijita hayatolewi kiholela bali yanafuata utaratibu fulani unaofumbata falsafa, mila na desturi za Kijita. Ingawa utafiti wa Nyanganywa (keshatajwa) ulihusu semantiki ya majina, uchunguzi wake wa taratibu za utoaji majina ulimwongoza mtafiti katika kufanikisha utafiti wake kuhusu kubainisha

vigezo vya utoaji wa toponemia za shule za msingi katika jamii ya Wamwimbi na Wamuthambi.

Kulingana na Azael (2013) majina katika jamii ya Wauru hutolewa kwa kutegemea hali ya kuzaliwa kwa mtoto, kama vile matatizo ama faraja alizokuwa nazo mama akiwa mjamzito au baada ya kujifungua. Mtafiti pia alibaini kuwa majina ya Kiuru yalitokana na mambo mbalimbali kama vile tabia ya mtoto, maumbile / mwonekano wa mtoto pindi alipozaliwa au wakati wa malezi, matukio mbalimbali ya kijamii, vipindi mbalimbali katika jamii na misingi ya imani na desturi ya Wauru. Maelezo haya yaliyotolewa na Azael (keshatajwa) yalisaidia kuchunguza vigezo vya utoaji wa toponemia katika jamii ya Wamwimbi na Wamuthambi. Aidha, mawazo yaliyotolewa na mtafiti huyu yalisaidia pakubwa katika utafiti huu kwani tafiti zote mbili zilichunguza vigezo vya kimaumbile na kijamii.

**MISINGI YA NADHARIA**

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Ujinaishaji iliyoasisiwa na kuendelezwa na wanaisimu Stuart, na wenzake, (2001) na Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi na Matini iliasisiwa na wanaisimu tekelezi katika bara Uropa kama vile Ruth Wodak, Norman Fairclough na Van Dijk (Wodak, 2001). Kutokana na Nadharia ya Ujinaishaji, utafiti huu uligundua kuwa majina ya mahali yalitokana na matukio ya jamii, mazingira ya kijiografia na shughuli zilizofanywa na wanajamii. Mihimili ya nadharia hii ilimsaidia mtafiti katika kuchanganua data ya utafiti. Mhimili wa mantiki ulimsaidia mtafiti kugundua mantiki iliyohusu utoaji wa majina ya shule msingi za Mwimbi na Muthambi. Maelezo yaliyotolewa na baadhi ya wahojiwa na hojaji kuhusu asili na maana ya toponemia hizi yalihitilafiana. Mtafiti alitumia mhimili wa mantiki kuamua maana iliyofaa kutwaliwa kutokana na maana zilizokinzana. Mhimili wa ukweli ulifaa mtafiti katika kubainisha maelezo ya toponemia yaliyofaa kulingana na maelezo yaliyotolewa na wahojiwa na hojaji. Kuna taarifa zilitolewa na Machifu kuhusu toponemia lakini wenyewe hawakuwa na uhakika nazo hivyo ilimbidi mtafiti kupata ukweli kutokana na mahojiano ya wazee.

Utafiti huu uligundua kuwa utoaji wa toponemia ni tukio la kijamii. Kwa hivyo mhimili wa utamaduni ulifaa katika kuonyesha kuwa toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi ziliakisi utamaduni wa jamii. Aidha, mhimili wa ufahamu kamilifu wa kitu au mtu ulikuwa muhimu kwa mtafiti kwani ilimbidi mtafiti kutafuta wazee wenye ufahamu wa toponemia kwa ili kupata maelezo sahihi. Katika mahojiano na wazee wakati mwingine mtafiti alielekezwa mahali ambapo angewapata wazee wenye ufahamu kamilifu wa toponemia. Mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi na Matini iliufaa utafiti huu katika kuchunguza vigezo vya utoaji wa toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi. Mhimili wa kubandika majina hasa ya kibaguzi ulisaidia kuonyesha namna sifa za kimaumbile, kiuchumi na kitabia zilivyochangia utoaji wa toponemia. Kwa jumla, nadharia hizi zilikuwa mihimili na dira ya kukitia na kuongoza matendo ya kijamii yaliyoakisi utoaji wa toponemia za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi.

**MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo katika kuchanganua data na kuwasilisha matokeo yake. Mtafiti aliteua sampuli kulingana na sifa za kuwa na uwezo wa kutoa data sahihi kulingana na lengo la utafiti huu. Sigh (2007), anasema kuwa, usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. **U**tafiti huu ulitumia sampuli ya kimaksudi ambayo iliteuliwa kwa kuchagua aina fulani ya watu ili kuwakilisha makundi maalum katika jamii (Kothari, 2004 na Mugenda, 2008). Watafitiwa 50 walichaguliwa: machifu 5 katoka kata 5 za eneo la Mwimbi na Muthambi, manaibu wa chifu 25 kutoka katika kata ndogo 25 za eneo hili. Sampuli hii ilichaguliwa kwa machukulio kwamba watawala hawa walikuwa wenyeji wa maeneo husika na wangekuwa na ufahamu kuhusu majina ya shule zilizo katika maeneo yao ya utawala. Kwa wale ambao hawakuwa na ufahamu huo, ilikuwa rahisi kwao kuuliza kutoka kwa wenyeji wa kata zao. Mtafiti aliteua sampuli ya wazee 20 wenye umri wa miaka 70 na zaidi kwa kutumia mbinu ya kimtandao. Umri huu ulitiliwa maanani kwa kuwa iliaminika kwamba wazee walikuwa na maarifa na tajriba ya kutosha kuhusu maana na michakato ya uundaji wa toponemia za Wamwimbi na Wamuthambi. Data katika utafiti huu ilikusanywa kwa njia ya hojaji na mahojiano. Mtafiti alitumia mbinu hizi mseto kwa lengo la kupata matokeo yaliyo bora kama walivyobainisha Best na Khan (1998), kwamba mbinu moja haitoshelezi katika kupata data zilizoaminika na kukubalika katika utafiti.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Utafiti huu ulibainisha vigezo kadha vilivyozingatiwa katika utoaji wa toponemia katika jamii. Vigezo hivyo ni pamoja na kuwepo kwa miti na mimea, toponimu, eponimu, kuwepo kwa viumbe mahali fulani, upatikanaji wa vitu maalum, matukio makuu katika jamii, shughuli za kijamii na majina ya ukoo**.** Hebu tuangazie vigezo hivyo.

**Kuwepo kwa miti na mimea**

Ilibainika kuwa utoaji wa majina ya shule za msingi za Mwimbi na Muthambi kwa kiasi kikubwa ulitokana na uwepo wa miti au mimea katika sehemu fulani. Kulingana na MhG 1, sio miti yote iliyotumika kutambulisha mahali bali miti ya kawaida iliyokuwa na matumizi maalum kwa jamii kama vile kutumika katika ujenzi wa nyumba, kutengeneza daraja, majani yake yaliliwa na mbuzi, watu walikutania hapo kwa shughuli maalum kama kutoa kafara au kubarizi. Toponemia zifuatazo za shule za msingi za Mwimbi na Muthambi

zilitokana na aina fulani ya miti au mimea iliyopatikana mahali fulani:

*Kathwana* ni jina la shule ya msingi iliyo mpakani mwa Mwimbi na Tharaka katika upande wa Mashariki. Kietimolojia jina hili lilitokana na kuweko kwa miti iliyoitwa *mithwana*. Miti hii ilipatikana kwa wingi katika eneo hili kuliko sehemu nyingine za Mwimbi, *Mithwana* ilizaa matunda yaliyoitwa *nthwana* yaliyokuwa na umbo la pilipili. Mbegu hizi zilitumiwa kutengenezea shanga ambazo zilitumiwa katika nyimbo za kiasili. Mahali ambapo shule hii imejengwa palijulikana kama Kathwana, kutokana na wingi wa *mithwana* iliyokuwapo. Hadi kufikia sasa mahali hapa panajulikana kwa jina hili ingawa miti hiyo ilikatwa na watu kwa ajili ya kilimo, uchomaji wa makaa na ujenzi.

*Mautini* ni jina la shule ya msingi iliyo katika kanda ya kielimu ya Kiera. Kigezo kilichotumiwa kutoa jina hili ni kuweko kwa mimea mingi iitwayo *mauti* ambayo ilimea katika sehemu hiyo. Mimea hii ililiwa na mbuzi na kondoo. Kulingana na MhK 1 na MhK 2, kichaka ambacho kilikuwa na mimea hii kilikuwa na rutuba kwa ajili ya kilimo hasa cha nafaka kama mawele na mtama. Shule hii ilijengwa mahali hapo baada ya kungoa mimea hiyo ya *mauti* iliyokuwa imeshikamana.

*Makuri* ni jina la shule ya msingi iliyo katika sehemu ya upande wa magharibi ya Mwimbi karibu na msitu wa mlima Kenya. Ni mahali penye baridi na mabonde mengi. Kulingana na MhK1, 2 na 4, kulikuwa na majani yaliyoitwa Makuri ambayo yalitoa harufu nzuri iliyovutia nyuki. Kwa sababu hii waliyatumia majani haya kuweka katika mizinga ili kuvutia nyuki. Kulingana na wahojiwa wa utafiti huu, Wamwimbi kutoka sehemu ya chini walienda huko ili kupata majani hayo kwa ajili ya mizinga yao. Kwa sababu ya wingi wa majani hayo mahali hapo palipewa jina Makuri.

Kigezo cha mti kilitumika kutoa jina la shule ya *Mukui*. Hii ni shule ya msingi iliyo katika kata ya Mugumango. Shule hii iko chini ya soko la Chiakanyinga kwenye barabara itokayo Katharaka kuelekea Kathwana. Jina la shule hii lilitokana na miti iliyoitwa Mikui. Kulikuwa na miti mingi ya aina hii katika sehemu hii. Umoja wa jina Mikui ni Mukui. Miti hii ilitumika sana katika ujenzi hasa kwa kupasua mbao na kukata boriti. Aidha, matawi yake yalitumika kama kuni. Miti hii ilikua sana mahali palipokuwa na maji au kandokando ya mto. Kulingana na MhG 4, shule hii ilijengwa karibu na Mukui mmoja uliokuwa mkubwa sana hivyo ikapewa jina Mukui.

*Mutiiguru* ni shule ya msingi iliyo katika kata ya Muthambi. Shule hii iko juu ya Kajiunduthi karibu na kiwanda cha majani chai cha Weru. Shule hii ilianzishwa na dhehebu la *Akorino*. Karibu na shule hii kuna vijiji viwili vya Kimuri na Kiathi. Kulingana na MhM 3, hapa ni mahali penye kilima kilichoaminika kilikuwa na mti mkubwa juu yake. Mti huo ulionekena kutoka mbali kama mti uliokuwa juu. Mandhari ya sehemu hii yalikuwa tambarare kadri mtu alivyoelekea kilimani na baada ya kilima hali ya utambarare iliendelea. Kulingana na MhM 3, kulikuwa na nyumba iliyojengwa mtini juu ili kutazama maadui wakikaribia. Kulikuwa na ngome mahali hapo iliyoitwa Mutiiguru. Kutokana na kuonekana kwa mti huo kwa mbali kama uliokuwa juu, mahali hapo paliitwa Mutiiguru kumaanisha mti ulio juu.

**Uzingatiaji wa toponimu**

Hii ni mbinu ya kuunda maneno, hususan majina ya mahali, kutokana na hali fulani ya kijiografia (Gichuru, 2010). Mbinu hii ni zalishi katika kuunda majina mbalimbali ya mahali. Katika lahaja ya Kimwimbi, baadhi ya toponemia za shule ya msingi zimeundwa kutokana na mbinu hii ya toponimi.

*Ndintune* ni jina la shule ya msingi iliyo katika kata ya Kaare upande wa Kaskazini Mashariki mwa mlima Kiera. Kulingana na MhK 3, mahali hapa palikuwa pa kutolea kafara kabla ya kuja kwa Wazungu. Maana ya jina hili ni nchi yenye udongo mwekundu. Mhojiwa huyu anaeleza kwamba eneo hili hadi sasa lina sehemu zenye udongo mwekundu. Udongo huu ulitumiwa kutengeneza vitu vya mapambo kama poda iliyoitwa *nondo* na kufinyanga vyungu. Kwa sababu ya aina hii ya udongo mahali hapo palirejelewa kama Ndintune.

Mwonekano wa nchi ulichangia uteuzi wa jina la Shule ya msingi ya *Kiera* lililotokana na mlima wa *Kiera* unaotambulika katika eneo la Mwimbi. Mlima huu unasifika kwa kuwa na aina ya udongo mweupe uitwao *ira* kwa Kimwimbi na chokaa kwa Kiswahili. Maana ya jina la mlima huu ni mahali penye ***ira.*** Mlima huu pia una miti ya kienyeji na mirungi itundwayo na watu kwa ajili ya mauzo. Aina hii ya chokaa ilitumiwa kujipaka sehemu za mwili wakati wa kuimba nyimbo za kienyeji. Kulikuwa na aina nyingine ya udongo uliokuwa mwekundu (nondo) uliotumiwa kama mapambo na wanawake. Wamwimbi walifanyia kafara kwenye mlima huu. Kwa hivyo shule hii ya msingi ilipewa jina Kiera kutokana na umaarufu wa mlima huu. Utoaji wa jina hili ulizingatia kigezo cha kimaumbile.

*Uthaini* ni shule ya msingi iliyo katika sehemu ya chini kabisa ya kata ya Kirumi. Mahali hapa ndipo mito miwili iitwayo Maara inapounganika karibu na mlima Kiera. Kulingana na MhG 7, Uthaini humaanisha mahali ambapo hapana rutuba. Ni mahali ambapo pana miamba, mawe, nyasi ndogo ndogo na changarawe. Taswira ya mahali hapa ni ya kutamausha kwani hakuna kilimo chochote kinawezekana hapo. Kwa Wamwimbi mahali kama hapo panajulikana kama *Ngaraini* ambacho ni kisawe cha *Uthaini*. Shule hii iliitwa Uthaini kutokana na hali na mwonekano wa mazingira ilimojengwa.

*Ntakani* ni jina la shule ya msingi iliyo katika lokisheni ya Kandungu katika barabara inayotoka Marima hadi Kathwana. Kulingana na MhG 8, eneo hili huwa na udongo unaoshikamana wakati wa mvua. Ni eneo ambalo halikupitika kwa sababu ya matope likilinganishwa na maeneo mengine jirani. Katika lugha ya Kimwimbi jina *ntaka* ni matope kwa hivyo mahali hapa paliitwa hivyo kutokana na wingi wa matope katika sehemu hii. Mahali ambapo barabara ni za matope huchukuliwa kuwa nyuma kimaendeleo. Watu wa sehemu hiyo hudunishwa na wengine waishio kwenye maeneo yaliyoendelea.

*Mbironi* hutumiwa kurejelea shule ya msingi iliyo katika kanda ya elimu ya Ganga. Shule hii iko katika kata ndogo ya Mukui katika lokisheni ya Mugumango kusini. Kulingana na MhG 9, shule hii imejengwa katika eneo linaloitwa Miraga. Jina lenyewe lilitokana na hali ya weusi (masizi) yaliyobaki katika sehemu hii baada ya kichaka kuchomwa. Eneo hili lilikuwa na miti mingi iliyoitwa miraga yenye miiba mikali na mikubwa. Watu wa eneo hili walichoma kichaka na miti kwa ajili ya kilimo. Uchomaji huu ulifanywa na vijana wa *Garu* lililokuwa hapo. Uchomaji wa kichaka ulifanywa pia ili kufukuza wanyama hatari kama simba, dubu na fisi waliokuwa wengi mahali hapo. Kwa sababu ya mbiro (masizi) yaliyosalia baada ya moto kupoa watu walipaita Mbironi yaani mahali penye masizi.

**Uzingatiaji wa eponimu**

Hii ni mbinu ya uundaji wa maneno kwa kuzingatia kigezo cha mtu maalum aliyevumbua au anayehusishwa na dhana fulani katika jamii. Dhana hiyo inaweza kupewa jina kwa heshima au kama kumbukumbu ya mtu maarufu ama mashuhuri. Suala la mbinu ya eponimu kutumika katika uundaji wa toponemia limeshadidiwa na maelezo ya Gichuru (keshatajwa) anapoeleza kuwa mbinu ya Eponimu ni maarufu katika kuunda majina ya barabara, mitaa, dawa, makampuni, taasisi na majina chapa ya bidhaa. Mifano ya majina yafuatayo inashadidia maelezo haya.

*Mwimbi* ni jina la shule maarufu ya kibinafsi katika kanda ya kielimu ya Chogoria. Mahali ambapo shule hii imejengwa hapaitwi Mwimbi ila shule tu ndiyo yenye jina hili. Kiasili shule hii imepata jina kutokana na jina linalotambulisha eneo kubwa linalomilikiwa na Wamwimbi. Kulingana na fasihi simulizi jina Mwimbi ni la mwanamume aliyeongoza kikundi kimojawapo cha Wameru walipotoka eneo lao la asili huko pwani ya Kenya. Mwanamume huyo aliitwa M‟Mwimbi aliyefika katika eneo hili na kuishi huko. Haya ni kwa mujibu wa MhK 1 na Mhk 3. Mwasisi wa shule hii aliita Mwimbi kwa ajili ya kujivunia uenyeji wa Mwimbi na kutunza kumbukumbu ya jina hilo. Kulingana na wahojiwa wa eneo hili, jina Mwimbi pia lina maana ya kujitegemea kutokana na kitenzi k*wiumba* (kujiweza) kinachozalisha nomino *mwiumbi* (anayejiweza) kwa hivyo kietimolojia jina la shule hii lilitokana na mtu aliyeitwa Mwimbi. Mwanamume huyo alikuwa na ndugu wengine waliobaki katika maeneo mengine ya Meru na kuwa chanzo cha makabila hayo kama Waimenti na Watharaka.

*Murunga* ni jina la shule ya msingi iliyo katika eneo la Mugumango chini ya soko la Mukui. Shule hii ilipewa jina kutokana na jina la mtu aliyeitwa Murunga. Kulingana na MhG 12, kuna kisasili kinachohusiana na upewaji jina la mahali hapa. Kulikuwa na mwanaume aliyeitwa Murunga na alikuwa hana mkono mmoja. Siku moja walipovamiwa na maadui, watu wote walitoka kupambana nao lakini maadui hao wakatokea upande mwingine na kumkuta Murunga peke yake. Murunga alipiga kelele ndipo wakatoroka lakini akambana mmoja wao kwa mkono mmoja. Alipiga kelele zaidi akisema,`Njooni nimemshika mmoja na mnajua nguvu za Murunga...‟ wenzake walifika na kumnusuru kisha maadui wakatokomea kwa kumwogopa Murunga. Kutokana na tukio hili mahali hapo paliitwa Murunga kutokana na jina la mwanamume huyo. Kwa sababu ya kisa hiki katika eneo la Mwimbi nzima kuna msemo utumiwao kama,‟Mainya ni ma Murunga‟ maana yake ni kukejeli hali ya kutokuwa na nguvu mtu anapofanya kazi ili wengine wasimtegemee au wamsaidie.

*Muthambi* ni jina la shule ya msingi iliyo katika tarafa ya Muthambi. Shule hii iko karibu na kituo cha kibiashara cha Marima umbali wa kilomita mbili kutoka kwenye barabara kuu ya Chuka-Meru. Jina Muthambi linarejelea eneo zima linalomilikiwa na jamii ya Wamuthambi ambao hupakana na Mwimbi upande wa Kaskazini, Chuka upande wa Kusini, Tharaka upande wa Mashariki na Upande wa Magharibi wamepakana na msitu wa mlima Kenya. Asili ya jina Muthambi ni mwanamume aliyeitwa Muthambi aliyeongoza jamii hii walipotoka pwani ya Kenya mahali palipoitwa *Mbwaa* (mahali pao pa asili). Maelezo haya ni kwa mujibu wa MhM 6, aliyesimulia kisasili cha uhamaji wa makundi ya Wabantu kutoka pwani ya Kenya na maeneo waliyoyamiliki. Kulingana naye, Wamuthambi walikuwa miongoni mwa makundi hayo ya Wabantu na walijumuisha koo nne mathalan: Aethimo, Asanyu ba Mburi na Bambiro, Aumu (Mbururi) na Akiini. Makundi haya ndiyo yalijumuisha Wamuthambi. Kwa hivyo, jina Muthambi linapotajwa huwa ni kumbukumbu ya asili na historia ya jamii hii.

*Jediel Kiraithe Academy* ni shule ya malazi ya mseto katika kata ya Kiera. Shule hii iko karibu na kituo cha kibiashara cha Magutuni kwenye barabara kuu itokayo Keria hadi Kathwana. Jediel Kiraithe alikuwa mtu mashuhuri katika serikali ya Kenya enzi za rais wa pili wa Kenya. Shule hii ilipewa jina hili kwa ajili ya ukumbusho wa Kiraithe Jediel. Shule hii ni ya umma ingawa jina la utambulisho ni la mtu binafsi. Walimu katika shule hii wameajiriwa na Tume ya Kuwaajiri Walimu ya Kenya (TSC). Kigezo cha utoaji

wa jina la shule hii ni kuwepo kwa mtu mashuhuri katika eneo inamopatikana.

**Kuwepo kwa viumbe mahali fulani**

Data za mahojiano na dodoso zilionyesha kuwa baadhi ya toponemia za shule za msingi za Mwimbi zilitokana na majina ya viumbe kama vile wanyama, ndege na wadudu. Viumbe hao walikuwa na sifa mahususi kama vile kushambulia mimea, kuwa wengi mahali fulani au walipitia eneo fulani.

*Nkangani* ni shule ya msingi iliyo katika kijiji kiitwacho Nkangani katika wadi ya Ganga. Jina hili lilitokana na jina *Nkanga* ambalo ni jina la ndege anayefanana na kuku. Ana mchanganyiko wa manyoya ya kijivu na meupe na kijipembe kichwani katikati. Ndege huyu alitegwa kwa ajili ya nyama na mayai kama alivyo kuku. Ndege hawa walikuwa hatari kwa kuchakura mbegu zilizopandwa. Walipatikana kwa wingi sana katika eneo hili na kusababisha watu kuacha eneo hili kuwa kichaka kwa kuhofia hasara ya kuchakuriwa mbegu na ndege hao. Walitembea kimakundi na kuitana kwa sauti ya ke!ke!ke! Baadhi ya watu waliwanasa na kuwafuga lakini wakatoroka baada ya kuwa wakubwa hasa majogoo yaliposikia sauti ya wengine vichakani. Sehemu hii iliitwa Nkangani kwa sababu ya Nkanga wengi waliokuwako.

*Kamachuku* ni jina la shule ya msingi iliyo karibu na Mitheru. Asili ya jina hili ni jina la Kimwimbi *nchuku* linalomaanisha kiota cha ndege. Maana nyingine ya jina *nchuku* ni ghala. Aidha, kulikuwa na ndege walioitwa *Machuku* waliojenga viota vyao kwenye miti ili waweze kulala baada ya kula mawele. Kwa sababu ya wingi wa ndege hawa na viota vingi walivyojenga mahali hapa palipewa jina Kamachuku kumaanisha mahali pa Machuku. Kigezo kilichotumika katika kutoa jina hili ni uwepo wa ndege walioitwa *Machuku* na viota vyao vilivyojulikana kama *nchuku* na wenyeji wa eneo hili.

Kigezo cha kuwepo kwa ndege kimetumiwa kutoa jina la shule ya msingi ya *Nturiri*. Shule hii iko katika barabara kuu itokayo Kieganguru kuelekea Kiairugu. Imejengwa baina ya soko la Nturiri na Behewa la Chogoria la Chuo kikuu cha Chuka. Jina Nturiri lilitokana na ndege walioitwa *Maturiki* katika hali ya wingi na *Ituriki* katika umoja. Kulingana na MhK 1, ndege hao walipatikana kwa wingi mahali hapo. Hawa ni ndege wenye umbo la njiwa lakini wakatofautiana kirangi. Walikuwa wenye rangi mchanganyiko wa samawati na kijani kibichi. Walipendeza kutazamwa kutokana na sura yao na hasa hali yao ya utulivu. Walipenda kutua juu ya mti na kushuka chini walipotaka chakula. Walipenda nafaka kwa hivyo walipatikana mahali kulikokuwa na mashamba ya nafaka kama mawele, mtama na mahindi. Ndege hao walinaswa na kuliwa na watu.

*Kianjagi* ni jina la shule ya msingi iliyo katika lokisheni ya Chogoria. Shule hii iko karibu na soko la Karaa kwenye barabara ya Chogoria-Karaa. Asili ya jina hili ni *Njagi* linalomaanisha Pundamilia. Maana yake ni mahali ambapo palikuwa na *Njagi* (pundamilia). Kulingana na MhG 1, eneo hili la Chogoria lilikuwa mbuga yenye miti mikubwa ambapo wanyama waliishi. Katika sehemu ambapo shule hii ya msingi ilijengwa kulikuwa na pundamilia wengi. Hii ndiyo sababu pakaitwa Kianjagi kumaanisha mahali penye *Njagi* (pundamilia) wengi.

**Upatikanaji wa vitu maalum**

Kwa mujibu wa data iliyopatikana kutokana na mahojiano ya ana kwa ana na wazee na vile vile dodoso, baadhi ya toponemia za shule za msingi zilitokana na vitu vilivyopatikana katika maeneo fulani. Mifano ya vitu hivyo ni mawe, milima, mito, mabonde, vilindi na vile vile vitu vilivyotengenezwa na binadamu.

*Makengi* ni jina la shule ya msingi iliyo upande wa Mashariki mwa soko la Magutuni. Shule hii iko karibu na kilima cha Kiera kwenye barabara itokayo Keria kuelekea Kathwana (Mji mkuu wa jimbo la Tharaka Nithi). Ilianzishwa na dhehebu la Katoleki ambalo lilisambaa kutoka upande wa Magharibi na kuanzisha shule na makanisa mengi katika sehemu hii ya Mwimbi. Asili na maana ya jina hili ni vitu vilivyometameta mfano wa vigae vya vioo vyepesi ambavyo vingeweza kubambuliwa. Mahali palipoonekana vigae vya namna hiyo palidhaniwa kuwa na madini mengine ya thamani. Kwa sababu hii Wazungu walichimba huko mlimani na kando kando wakitafuta dhahabu. Kutokana na shughuli hiyo ya kuchimba, vigae vingi vya aina mbalimbali vilisambaa kila mahali katika eneo hilo la karibu na mlima. Jina Makengi lilitokana na wingi wa vigae hivyo vilivyotapakaa karibu na eneo lililojengwa shule ya Makengi.

Shule ya msingi ya *Kanoro* inapatikana katika makutano ya njia itokayo Katharaka na inayotoka Marima zikielekea Kathwana. Shule hii iko karibu na kivuko cha Muthandara katika mto Maara. Asili ya jina hili ni kitendo cha kunoa yaani kutia makali vyombo kama vile visu, panga, jembe, shoka au vigumba vya mikuki. Vifaa vilivyotumika kutilia makali viliitwa Manoro kwa wingi na Inoro katika umoja. Yalikuwa ni aina ya mawe ambayo yalipatikana kwa wingi katika sehemu hii na watu kutoka sehemu mbalimbali za Mwimbi walienda kuyaokota ili kuyatumia nyumbani kwao.

*Kathangawe* ni shule ya msingi iliyo katika wodi ya Mitheru jimboni dogo la Maara. Lugha ya wakaaji wa eneo hili ni Kimwimbi ingawa kiutawala wamo katika eneo la Muthambi. Jina la shule hii limetokana na jina *ithangawe* katika hali ya umoja na *Mathangawe* katika wingi. *Mathangawe* ni aina ya mawe mekundu yaliyo magumu sana. Mawe hayo

yalitumiwa kuchongea kinu cha kusagia uji. Yalitumiwa pia kunolea visu na mikuki. Kulingana na MhM 7, eneo hili ambamo shule imejengwa palikuwa na mawe mengi ya aina hii. Kwa sababu ya sifa hii mahali hapa paliitwa Kathangawe ambalo ni udogo wa mathangawe.

Shule ya msingi ya *Kajiunduthi* inapatikana katika barabara kuu inayotoka Chuka hadi Meru. Shule hii iko karibu na mto Maara na vile vile soko la Marima. Wakoloni walijenga kambi yao katika sehemu hii. Wazee wengi waliohojiwa hawakujua asili na maana ya jina hili. Kulingana na MhM 4, jina hili lina asili ya Kikamba. *Nduthi* ni chuma kilichotumiwa kugongea vyuma wakati wa ufuaji vyuma. Kuna Wamwimbi waliokuwa wakifua vyuma katika sehemu hii. Wakamba walipokuja sehemu hii kwa ajili ya biashara walisema hapo ni mahali pa *Nduthi* kwa sababu chuma hicho kilitumiwa kufulia chuma katika sehemu hii. Watu wa mahali hapo walianza kupaita Kajiunduthi yaani mahali pa *Nduthi*.

**Matukio makuu katika jamii**

Majina mengine ya shule za msingi yalitolewa kutokana na mambo yaliyotokea katika jamii kama vile ya kiuchumi, kiutawala au ya kitamaduni.

*Kajiongo* ni shule inayopatikana karibu na soko la Marima kukabiliana na mto wa Nithi. Jina la asili la eneo hili lilikuwa Kithitu kutokana na msitu uliokuwa katika sehemu hiyo.Utawala wa kikoloni ulijenga kambi mahali hapo katika kipindi cha vuguvugu la Maumau. Watu waliouawa huko msituni na askari wa Kikoloni na Waafrika waliowaunga mkono, Maiti zao zilipelekwa katika kambi ili kuzikwa mahali palipotengwa. Kwa sababu ya makaburi ya watu waliozikwa mahali hapo palijulikana kama *Kajiongo* kwa maana ya mahali pa vichwa. Hii ni kwa sababu kulikuwa na mafuvu mengi ya watu. Shule ilipojengwa mahali hapo ilipewa jina Kajiongo. Matamshi ya jina hili na mofolojia yake inaonyesha kuwa jina hili ni la Kimwimbi ingawa linapatikana katika eneo la Muthambi.

Neno *Chogoria* lina asili yake katika kipindi cha ukoloni ambapo wamishenari kutoka Uingereza walifika katika eneo la utafiti kwa minajili ya kueneza injili pamoja na elimu. Kulingana na MhC 11, neno Chogoria lilitokana na kirai *kunyogoria mauntu,* yaani kuvuruga au kuharibu mambo. Mmishenari aliyeitwa Dkt. Clive Irvine alikuwa na mipango mizuri ya kimaendeleo ya kukuza jamii kama vile kuleta huduma ya matibabu na masomo. Watu wa eneo hili hawakuwa tayari kumuunga mkono bali waliharibu mipango hiyo. Viongozi wao waliudhika na kuwaita *anyogoria a mauntu* (watu wanaoharibu mambo). Kwa sababu Dkt. Clive Irvine hangeweza kutamka *anyogoria* akasema, "nyinyi ni a Chogoria", hivyo basi watu wa eneo hili wakaanza kuitwa Wachogoria na mahali pao pakaitwa Chogoria. Inaaminika kuwa watu wanaoishi katika eneo la Chogoria walitokana na mwanamke aliyeitwa Mwanjora.

*Mutindwa* ni jina la shule ya msingi iliyo katika kata ya Chogoria mahali kujulikanako kama Mutindwa wa Mbogori. Kiasili shule hii iliitwa Mutindwa wa Mbogori kutokana na Chifu Mbogori aliyetawala kabla na baada ya uhuru. Chifu Mbogori alitawala eneo kubwa la Mwimbi na Muthambi. Maana ya jina Mutindwa ni mahali pa kushinda au kukaa. Jina hili lilitumika kurejelea sehemu hii kwa sababu watu kutoka maeneo mbalimbali walienda na kushinda hapo kwa Chifu Mbogori. Watu wengi walienda kwa Chifu kwa ajili ya kutatuliwa kesi au masuala mbalimbali ya kiutawala. Kulingana na MhG 1, umati wa watu kutoka sehemu nyingi za Mwimbi na Muthambi walishinda katika kambi ya Chifu Mbogori ili kutatuliwa matatizo yao. Kutokana na hali hiyo ya kukaa mahali hapo kwa Chifu pakaitwa Mutindwa wa Mbogori, jina ambalo limedumu hadi sasa. Iwapo mtu angekwenda na kukawia sana mahali fulani Wamwimbi walizua msemo, *Kagwatwika Mutindwa?* Yaani kwani kumekuwa Mutindwa?

**Shughuli za Kijamii**

Kulingana na data iliyopatikana kutokana na mahojiano na dodoso, jamii za Mwimbi na Muthambi zilijinaisha mahali kutokana na shughuli mbalimbali zilizofanywa na wanajamii. Shughuli hizo zingekuwa za kiuchumi, kitamaduni au za kidini. Toponemia zifuatazo za shule za msingi zinashadidia maelezo haya.

*Kanini* ni shule ya msingi iliyo karibu na mlima Kiera. Ilianzishwa na kanisa la ACK mnamo miaka ya sabini. Imejengwa Katika makutano ya njia itokayo Magutuni na inayotoka Kieni zikielekea katika upande wa Tharaka kupitia soko la Kaare. Shule hii iliitwa Kanini kwa sababu ilianzishwa na kikundi cha wanawake cha kanisha la ACK kilichojitambulisha kama Kanini. Kijiografia shule hii iko katika eneo linaloitwa Rurama kutokana na miti iitwayo mirama iliyokua huko kwa wingi. Neno Kanini humaanisha kidogo. Kikundi cha wanawake kilikuwa kidogo yaani kilikuwa na wanachama wachache kilipoanzishwa. Kwa hivyo udogo hapa unarejelea uchache wa wanachama.

Shule ya msingi ya *Kamwangu* inapatikana katika kata ndogo ya Kamwangu. Jina hili linatokana na wimbo wa kitamaduni uitwao Mwangu. Uliimbwa na vijana wa kiume na wa kike. Vijana hao walifyeka kichaka kilichokuwa mahali ambapo shule hii imejengwa ili kutengeneza uwanja wa kuimbia. Vijana walioolewa majuzi pia wangeweza kushiriki wimbo huu lakini wangeondoka mapema ili kufika nyumbani kushughulikia watoto. Kulikuwa na msemo wa Kimwimbi kuwa, *Tukiina mwangu ndi mwari indi twenuka ndi muka* „tukiimba *mwangu* mimi ni msichana lakini nikienda nyumbani ni mwanamke‟ wimbo huo uliimbwa mwezi wa septemba baada ya kunywa uji, kula mbaazi na ndizi mbivu.

*Kalewa* ni shule ya msingi inayopatikana katika eneo la Chogoria. *Kalewa* linatokana na jina *lewa* linalomaanisha vijana waliotahiriwa. Kulingana na utamaduni wa Wamwimbi, vijana hao waliwekwa katika sehemu mbalimbali mahsusi ili kulinda usalama. Vijana hao pia walikutanika mahali fulani kwa ajili ya kujiburudisha kwa nyimbo za kiasili. Waliletewa chakula mahali hapo. Wanawake hawakukubaliwa kuwa mahali hapo. Shule hii iliitwa Kalewa kwa sababu ndipo (lewa) vijana walipokutana.

Kwa mujibu wa MhG 1, jina *Ndumbini* linatokana na jina Ndumbi lililo na maana tatu. Kuna *Ndumbi* ambacho ni aina ya chondo kilichojazwa na kusimikwa mashuke ya mawele au mtama ili kuruhusu nafaka zaidi kutiwa ndani. Aina nyingine ya Ndumbi ni mtungo wa aina ya kata iliyosimikwa manyoya marefu ya ndege. Kifaa hiki kilitumiwa kama maleba katika nyimbo za kiasili. *Ndumbi* ya tatu ni aina ya nyumba ya mviringo yenye paa la umbo la pia iliyoketishwa lenye kijiti kilichochongoka katikati. Asili ya jina la shule ya msingi ya Ndumbini ni mtungo uliotiwa nakshi za manyoya ya ndege zilizotengenezwa katika sehemu hiyo. Watu fulani katika sehemu hii walikuwa stadi katika utengenezaji wa ndumbi na kuwauzia watu wa maeneo mengine. Kwa sababu ya upatikanaji wa vitu hivyo katika sehemu hii, watu walianza kupaita mahali hapo Ndumbini.

*Maguma* ni shule ya msingi ya zamani katika soko la Magutuni. Imejengwa chini ya mlima Kiera. Mdhamini wa shule hii ni dhehebu la Wakatoleki waliokuwa Wamisheni wa kwanza katika eneo hili. Jina Maguma linatokana na kitenzi kugomana chenye maana ya kukutana. Kietimolojia, jina Maguma lilitokana na kitendo cha wazee wa *Njuri* ncheke kukutania hapo ili kufunza vijana mambo ya *Njuri*. Watu walileta wanyama hapo ili kutolewa kafara. Mahali hapo ndipo palikuwa na *Garu* kubwa sana kuliko zote katika sehemu hii ya Mwimbi.Vijana waliotahiriwa kutoka sehemu zote za Mwimbi walikutana hapo ili kufunzwa kuimba. Hapa ndipo wengine waliweza kupata wasichana wa kuoa. Jina Maguma hutumika kurejelea mahali tu ambapo shule imejengwa kwani vijiji vinavyopazunguka vina majina tofauti. Jina la shule ya msingi ya Maguma kwa hivyo, limetokana na kitendo cha kugomana kinachozalisha jina Magomano linalotamkwa Maguma.

Kulingana na MhK 1, jina Kieganguru lilitokana na kitendo cha kwigagura chenye maana ya kustaftahi. Alieleza kuwa katika sehemu hii kulikuwa na kambi kubwa ambapo watu kutoka sehemu mbalimbaii za Mwimbi walikutana. Hapo ndipo wazee wa baraza la Njuri ncheke walikutana ili kutatua na kujadiliana kuhusu maswala ya maendeleo.Wazee kutoka *Garu* (Ikulu) mbalimbali za Mwimbi walikutana hapa asubuhi mapema. Wengine waliokutania hapo ni wafanya biashara za kubadilishana bidhaa. Makundi haya yalifika hapo mapema na kupata kiamsha kinya hapo. Walisema, hapo ndipo *tukegagurira* yaani hapo ndipo tutakapostaftahi. Kwa sababu ya mazoea hayo mahali hapo pakajulikana kama Kieganguru kutokana na neno *kuigagura*.

*Kiriani* ni shule ya msingi iliyo katika lokisheni ya Chogoria kwenye barabara kuu itokayo Nairobi hadi Meru. Shule hii imedhaminiwa na dhehebu la P.C.E.A. Inapatikana karibu na soko la Kiriani baada ya mwinuko wa mto Maara. Kulingana na MhG 10, jina Kiriani linatokana na jina *Kiria* linalomaanisha kichwa kilichonyolewa kabisa. Kulikuwa na mwanamke mkongwe aliyewanyoa watu nywele. Watu wengi walikwenda kwa mwanamke huyo kunyolewa wakati wa tohara au baada ya kina mama kujifungua. Jina Kiriani liliibuka kutokana na kauli za watu kuwa naenda kunyolewa *kiria* yaani kunyolewa kabisa. Kulingana na mpito wa wakati mahali hapo palirejelewa kwa jina Kiriani.

**Majina ya ukoo**

Kwa mujibu wa Kamusi sanifu ya Kiswahili, ukoo ni uhusiano wa watu wa kitovu au aila moja. Watu wa ukoo mmoja huwa na ukruba na uhusiano shakiki kuliko wasio wa ukoo mmoja. Toponemia kadhaa katika eneo la Mwimbi na Muthambi zimeundwa kwa kuzingatia kigezo cha ukoo.

*Ukuruni* ni jina la shule ya msingi ya umma iliyo katika wadi ya Ganga. Shule hii imepewa jina kutokana na mbari ya Akuruni. Watu wa mbari hii wanamiliki eneo kubwa kutoka Ikumbo hadi soko la Kibura. Mashamba katika sehemu hii yalikuwa ya mbari hiyo ya Akuruni. Kutokana na jina la ukoo la *Akuruni* ndipo Ukuruni lilipatikana. Jina *ukuruni* humaanisha mahali ambapo mimea hukua haraka. Katika sehemu hii vyakula hukua haraka ikilinganishwa na sehemu nyingine za nyanda za juu za Mwimbi.

*Kiini* ni Shule ya msingi inayopatikana katika eneo la Muthambi lililo baina ya mto Nithi na mto Tungu. Asili ya jina la shule hii ni ukoo wa Akiini. Kulingana na MhM 3, kulikuwa na mtu mashuhuri wa ukoo wa Akiini aliyeishi mahali hapo. Hii ndiyo sababu shule hii ilipewa jina hilo.

## HITIMISHO LA UTAFITI

Utafiti huu ulichunguza vigezo vya utoaji wa toponemia katika jamii za Wamwimbi na Wamuthambi. Mtafiti aliongozwa na lengo mahsusi na swali la utafiti. Matokeo yalionyesha kuwa kulikuwa na vigezo vilivyoongoza utoaji wa toponemia katika jamii kama vile maumbile ya mahali, vitu vilivyopatikana mahali fulani kama miti au mimea, wanyama, ndege na wadudu. watu mashuhuri walioishi mahali fulani na matukio makuu katika jamii.

## ORODHA YA VIFUPISHO

MhC: Mhojiwa kutoka sehemu ya Chogoria
MhG: Mhojiwa kutoka sehemu ya Ganga

MhK: Mhojiwa kutoka sehemu ya Kiera
MhM: Mhojiwa kutoka sehemu ya Muthambi
C.C.M: Church of Scotland Mission
E.A.P.C: East Africa Pentecost Church
P.C.E.A: Presbyterian Church of East Africa
N: Nomino
V: Vivumishi

**MAREJELEO**


- Azael, R. (2013*). Maana ya Majina ya Asili Katika Jamii ya Kiuru.*Tasnifu ya M.A Kiswahili (isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Dae es Salaam.
- Baitan, B. (2010).*Morphosemantic Analysis of Ruhaya Person Names.*(Unpublished) M. A Dessertation, University of Dar es Salaam.
- Best, J., & Khan, J. (1998). *Research in Education*, New Jersey, Eaglewood Cliffs.
- Buberwa, A. (2011). *Viambishi ngeli katika nomino za pekee: mifano katika majina ya Kihaya,* Kiswahili, Juz. 74. Kur. 41 – 48.
- Crystal, D. (1987). The Encyclopedia of Language. Cambridge: CUP.
- Gichuru, T. (2010). *Uchanganuzi wa Nomino Ambatani za Kiswahili: Mtazamo wa Mofolojia Leksia*, Tasnifu ya Umahiri, Haijachapishwa. Chuo kikuu cha Kenyatta.
- Guma, M. (2001). The Cultural Meaning of Names among Basotho of Southern Africa. *Nordic Journal of Africa Studies* 10(3): 265 – 279.
- Habwe, J., Karanja, P. (2007). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Kahigi, K. (2007). Ujanibishaji wa office 2003 na Windows XP kwa Kiswahili sanifu katika *Kioo cha Lugha*. *Jarida la Kiswahili na Fasihi. Jizuu la 5. Idara ya Kiswahili,* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kihore, P., & Wenzake, (2004). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu:* Sekondari na Vyuo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.
- Kothari, C. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques,* New Delhi: New Age International (P) Ltd.
- Manyasa, J. (2009). *Investigating the Basis of Naming people in Kisukuma*, Unpublished, M.A Dessertation, University of Da es salaam.
- Masanja, N. (2019). Uchunguzi wa kisemantiki wa majina ya asili katika koo za Ginantuzu.Tasnifu ya uzamifu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Massamba, D. (2004). *Sarufi misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Nairobi Phoenix Publishers
- Mphande, L. (2006). *Naming and Linguistics Africanism in African- American Culture*. New York:Ohio University.
- Majapelo, P. (2009). ‟ Namna ngeli zinavyosaidia kuunda majina ya watu‟ (unpublished) M.A Dissertation. University of Dar-es-salaam.
- Mugenda, M., &Mugenda, G. (2000). *Research Methods: qualitative and quantitativeapproach.* Acts press Nairobi.
- Musere, J. (2010). *African Personal Names. The Great Lakes Areas.* Lantham MD: Scare Scrow Press.
- Musymi, D. (2011). Maana za majina ya Watu katika jamii ya Wakamba, Tasnifu ya shahada Ya uzamili, Kenyatta University *Bantu Names.* Kiswahili (61):28-49. 190 New Age International Publishers. Ltd
- Mwenamseke, F. (2011). *Uainishaji wa ngeli katika lugha ya Kibena.* Tasnifu ya Uzamili (isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Nyanganywa, M. (2013). Uchunguzi wa Kisemantiki na Taratibu za Utoaji wa Majina ya Kijita.Tasnifu ya M.A Kiswahili (isiyochapichwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Raybum, A. (2010). *Place names.* The Canadian Encyclopedia- Historical- Dominion.
- Rye J, (2006). *A popular Guide to Norfolk Place names.* Guist Bottom: Larks Press.
- Rubanza, Y. (2000). The Linguistic Creativity of Haya Personal Names.*Journal of Institute of Kiswahili Research*, Vol. 63, TUKI, Dar es Salaam
- Rugemalira, J. (2009). *A Grammar of Runyambo*, Dar es Salaam: Language of Tanzania Project, University of Dar es salaam.
- Werner-Lewis, M. (2003). *Central Africa in the Carribean Transcending,Time,Transforming Culture,* University of the WestIndies Press; Jamaica.
- Stuart, M. na wenzake. (2001). *Different types of dictionaries* Grin Verlang.
- Wodak, R. (2001). *Methods of critical Discourse analysis*, Sage publications London.


**Cite This Article:** David Micheni Mutegi, Allan Mugambi, Timothy Kinoti M‟Ngaruthi (2022). Ubainishaji wa vigezo vya Utoaji Wa Toponemia katika Jamii: Mfano kutoka Jimbo Dogo la Maara nchini Kenya. *East African Scholars J Edu Humanit Lit*, 5(9), 176-184.